



United Nations  
Educational, Scientific and  
Cultural Organization

KITENGO CHA TURATHI ZISIZOGUSIKA  
www.unesco.org/culture/ich



MEI 2007

n° 6

ISSN 2071-7784

## Maafikiano 2003

KUIDHINISHWA NA MATAIFA KUFIKIA  
APRIL 12, 2007

- 1 ALGERIA
- 2 MAURITIUS
- 3 UJAPANI
- 4 GABON
- 5 PANAMA
- 6 UCHINA
- 7 JAMHURI YA AFRIKA YA KATI
- 8 LATVIA
- 9 LITHUANIA
- 10 BELARUS
- 11 REPUBLIC OF KOREA
- 12 USHELISHELI
- 13 JAMHURI YA KIARABU YA SYRIA
- 14 UMOJA WA MILKI ZA KIARABU
- 15 MALI
- 16 MONGOLIA
- 17 CROATIA
- 18 EGYPT
- 19 OMAN
- 20 DOMINICA
- 21 HINDI
- 22 VIET NAM
- 23 PERU
- 24 PAKISTANI
- 25 BHUTAN
- 26 NIGERIA
- 27 ICELAND
- 28 MEXICO
- 29 SENEGAL
- 30 ROMANIA
- 31 ESTONIA
- 32 LUXEMBOURG
- 33 NICARAGUA
- 34 CYPRUS
- 35 UHABESHI
- 36 BOLIVIA
- 37 BRAZIL
- 38 BULGARIA
- 39 HUNGARY
- 40 JAMHURI YA KIISLAMU YA IRAN
- 41 JAMHURI YA MOLDOVA
- 42 JORDAN
- 43 SLOVAKIA
- 44 UBELGIJI
- 45 TURKEY
- 46 BUKINI
- 47 ALBANIA
- 48 ZAMBIA
- 49 ARMENIA
- 50 ZIMBABWE
- 51 CAMBODIA
- 52 JAMHURI YA YUGOSLAV YA MAKEDONIA YA AWALI
- 53 MOROCCO
- 54 UFARANSA
- 55 CÔTE D'IVOIRE
- 56 BURKINA FASO
- 57 TUNISIA
- 58 HONDURAS
- 59 SAO TOME AND PRINCIPE
- 60 ARGENTINA
- 61 UFILIPINO
- 62 BURUNDI
- 63 PARAGUAY
- 64 JAMHURI YA DOMINICA
- 65 GUATEMALA
- 66 HISPANIA
- 67 KYRGYZSTAN
- 68 MAURITANIA
- 69 UGIRIKI
- 70 LEBANON
- 71 NORWAY
- 72 AZERBAIJAN
- 73 URUGUAY
- 74 SAINT LUCIA
- 75 COSTA RICA
- 76 VENEZUELA

## “Turathi-Hai: Kuchunguza Zisizogusika” Maonyesho ya Picha UNESCO Paris

Mnamo Aprili 13, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO Koïchiro Matsuura, akisaidiwa na Balozi Seiichi Kondo ambaye ni mjumbe wa Kudumu wa UNESCO kutoka Ujapani, alifungua maonyesho ya picha kuhusu “Turathi-Hai: Kuchunguza Zisizogusika.” Picha hizo zilikuwa zimeonyeshwa hadharani kwenye ua unaozunguka makao makuu ya UNESCO mjini Paris.

Maonyesho hayo yalibainisha uanuwai wa uhai wa turathi zetu zinazoishi ulimwenguni. Yalionyesha zaidi ya picha za rangi mia moja kubwa za watu mbalimbali ulimwenguni wakifanya maigizo ya kitamaduni na desturi za kijamii: tokea usanii wa muziki, ngoma na uigizaji hadi matambiko, masimulizi ya kiasili na kazi za mikono. Matini zilizowekwa upapi zilisisitiza umuhimu wa kuhifadhi turathi zetu za tamaduni zisizogusika, pamoja na kueleza shughuli za UNESCO katika eneo hilo. Maonyesho haya ni sehemu moja ya mikakati ya UNESCO kubainisha wazi kwa ulimwengu hifadhi ya turathi za tamaduni zishizo – na muhimu zaidi – kwa Maafikiano ya 2003.

Kutoka mwaka wa 2001 hadi 2005, UNESCO ilitangaza takriban Vito vya Thamani 90 vya Mapokezi ya Mdomo na Hifadhi za Turathi Zisizogusika za Kibinadamu. Shughuli za UNESCO katika mawanda ya hifadhi hizi zilifikia kilele katika kukubali, kukuza na kuidhinishwa kwa Maafikiano ya Turathi Zisizogusika ya 2003. Maonyesho ya sasa ambayo pia yanaweza kupatikana katika wavuti ([www.unesco.org/culture/ich/en/expo/](http://www.unesco.org/culture/ich/en/expo/)) yanaonyesha picha za Vito hivyo 90 vya thamani, zikiwemo sherehe zinazopendwa huko Bolivia na Ubelgiji. Maigizo ya kirasimi ya kijapani na kihindi au uimbaji wa sauti nyingi kutoka Jamhuri ya Afrika ya Kati, Georgia na Albania. Vito vyote 90 vya Thamani vitawekwa pamoja kwenye Orodha ya Vito Wakilishi vya Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Kibinadamu iliyoanzishwa chini ya Maafikiano ya 2003. Maonyesho haya yamekita katika mambo ya zamani yanayoonyesha turathi zisizogusika kama zinavyotam-

buliwa chini ya mpango wa Vito vya thamani, yote ambayo yaliishia katika kuanzishwa rasmi kwa Maafikiano ya mwaka wa 2006. Mpango huo unatazamia kutekelezwa zaidi kwa Maafikiano hayo, na hivyo kufungua ukurasa mpya katika kulinda turathi za tamaduni zisizogusika ulimwenguni kote.

Chimbuko la picha hizo lina uanuwai kama yalivyo yale yaliyomo katika picha hizo. Zingine zilipigwa na wataalamu wa kupiga picha ilhali zingine zilipigwa na watafiti pamoja na watu wanaofanya kazi katika mawanda ya turathi za kitamaduni. Zingine zilipigwa na weledi wanaotekeleza kazi hizi pamoja na wanajamii. Maonyesho ya Paris yataendelea hadi Novemba 30, 2007 na yanafanyika kwingine pia kama vile Abu Dhabi katika Umoja wa Milki za Kiarabu, na hivi karibuni yatafanyika Uchina (Tazama kisanduku cha habari katika ukurasa unaofuata).

© David Steinhilber



Papi za picha mbeke ya lango la UNESCO.

## Tahariri

Uzingativu wa Maafikiano ya Turathi Zisizogusika katika uhifadhi umechochea taaluma mbalimbali na taasisi kutathmini upya shughuli zao. Kwa mfano, makavazi nyingi zimeanzisha desturi nzuri za kuwasilisha turathi zisizogusika kama turathi zinazoishi na kwa njia hii, kuvipa uhai vitu ambavyo zamani vilithaminiwa kama vitu vya kisanaa tu, huku vikihusisha jamii zinazoumba na kutumia vitu hivyo. Wazo la ‘kuishi’ ni muhimu kwa Maafikiano ambayo yanaeleza ulinzi kama “hatua zinazolenga katika kujitegemea kwa Turathi za Tamaduni Zisizogusika.” Baadhi ya hatua za ulinzi zilizofanuliwa kwenye Maafikiano, ‘ulinzi wa kimaandishi’ ndio unaojitokeza zaidi. Kwa hivyo, swali ni kwa jinsi gani turathi zitahifadhiwa

kwa njia ya maandishi ili kuchangia kikamilifu ulinzi huu? Au kwa njia nyingine, ni kwa njia gani tutatumia yale yaliyoandikwa kwa madhumini ya kuhifadhi?

Toleo hili la *Messenger* linajadili mkutano uliofanywa kushughulikia maswala haya na kutoa maelezo ya kitajriba kutoka katika nchi mbalimbali. Kuhifadhi kwa njia ya maandishi kunaweza pia kuchangia katika malengo mengine ya Maafikiano, kwa mfano, kujua zaidi kuhusu Turathi za Tamaduni Zisizogusika, na kuimarisha utambuzi wa watu kuzihusu. Katika muktadha huu, toleo hili la *Messenger* linatoa vielelezo vya maonyesho ya picha ambazo sasa zimetandazwa kwenye nyua za jumba la UNESCO liitwalo Fontenoy, pamoja na Kituo cha Habari kilichoingwa hivi karibuni ili kusaidia kutekeleza Maafikiano hayo.

Rieks Smeets, Kitengo cha Turathi Zisizogusika

Upapi wa picha ukionyesha sherehe za Barranguilla, Colombia, na jengo kuu la UNESCO likiwa nyuma.



© Javali Thierry

## Mkutano wa Wataalamu kuhusu Hifadhi za Maandishi na Nyaraka zihusuzo Turathi za Tamaduni Zisizogusika

Tarehe 12-13 Januari 2006, wataalamu wa kimataifa 24 walikutana Paris kujadili maswala muhimu yaliyohusu kuandika na kuhifadhi nyaraka za turathi za tamaduni zisizogusika kulingana na Maafikiano ya 2003. Wataalamu hao walizingatia masuala ya kisheria na kimaadili kuhusu uandikaji unaofanywa na wanajamii na ukuzaji wa umilisi huu miongoni mwao. Walizingatia pia haja ya kuhifadhi upya maandiko ya zamani kwa jamii. Washiriki waliripoti kuhusu njia mpya zenye matokeo ya kutumainisha kwa kuzingatia miradi mbalimbali ulimwenguni ambayo inapendekeza matumizi ya hifadhi za kimaandishi za Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Hii ni kwa minajili ya kuhakikisha uhuishaji na uendelezaji wa desturi na masimulizi kupitia kwa maandishi. Wataalamu walikubaliana kwamba lazima jamii zihusishwe katika hatua zote za kurekodi na kuandika turathi zao, na wawe wafaidi wa kwanza.

Aidha, walisisitiza usambazwaji wa habari kuhusu Turathi za Tamaduni Zisizogusika kwenye vyombo vya habari na kuingiza habari hizo kwenye mitaala ya shule kama njia ya kuinua kiwango cha utambuzi wa umuhimu wa turathi hizi. Walijadiliana juu ya tajriba katika uhifadhi wa kimaandishi unaohusisha jamii, na uwezekano wa shughuli hiyo miongoni mwa wanajamii. Kadhalika, walijadili juu ya mafunzo yatakayohitajika ili kuzihusisha jamii na makundi moja kwa moja kwa ajili ya kuwawezesha baadaye kuamua jinsi ambavyo wangependa sheria zao za kiasili na desturi kuheshimiwa. Maafikiano yenyewe yanahimiza jamii na makundi yahusishwe kwa karibu katika kutekeleza hatua za kulinda turathi.

Wakati wa mkutano, wataalamu walihimiza kuanzishwa kwa ushirikiano na uhusiano ambao unaweza kuvyaza mienendo chanya miongoni mwa jamii, taasisi maalumu, mashirika ya kimataifa, mamlaka za kitaifa na kimaeneo. Miundo ya ushirikiano kama hii inaweza kuwafungulia njia za kuweza kufikia turathi zao ambazo kwa sasa hazifikiki kwa jamii hizo. Aidha, itaweza kuanzisha njia tofauti za kushirikiana na kupata maandiko ya turathi yaliyo nje ya maeneo yao. Njia hii tayari imeonyesha kufaulu kwa baadhi ya jamii kurudishiwa tena baadhi ya turathi zao na kuzitumia katika shughuli za kuhifadhi. Ripoti yote ya mkutano inaweza kupatikana katika wavuti wetu. Vielelezo mahsusi kutoka Hungary, Ufilipino, Viet Nam na Papua New Guinea vimefafanuliwa hapa katika toleo hili la *Messenger*.

### Maonyesho ya Picha ya UNESCO katika Umoja wa Milki za Kiarabu na Uchina

Tonyesho la picha “Turathi- Hai: Kuchunguza Zisizogusika” ambalo hivi sasa limetandazwa UNESCO mjini Paris linasafiri. Hivi majuzi lilihusishwa kama tukio ambatanishi katika mkutano wa kwanza wa kimaeneo uliohusisha mataifa ya Kiarabu juu ya kuhifadhi turathi za tamaduni zisizogusika (Machi 31-Aprili 3 2007), ambao ulifanyika wakati wa maonyesho ya vitabu ya Abu Dhabi. Maonyesho haya yatakuwa katika eneo litwalo *Intangible Cultural Heritage Theme Park* huko Chengdu, Uchina, kama sehemu ya sherehe za kimataifa za Chengdu kuhusu Turathi za Tamaduni Zisizogusika (Mei 23 – Juni 10 2007). Kuzinduliwa rasmi kwa bustani hiyo iitwayo *Theme Park* kunaenda sambamba na kikao cha kwanza kisi-chokuwa cha kawaida cha Kamati ya serikali za nchi ambacho kitafanyika Chengdu kuanzia tarehe 23 hadi 27 Mei, 2007.

## Kuhifadhi Kimaandishi Turathi za Tamaduni Zisizogusika: Mifano Minne

### HUNGARY: Kuandikwa kwa Turathi za Kimuziki

Baada ya zaidi ya miaka 100 ya utafiti na uandishi, hifadhi kubwa ya rekodi za muziki, zikiwemo picha, sauti na picha zilizonaswa, pamoja na maandishi ya muziki wa kiasili yamekusanywa katika maakaba ya *East European State*. Maafikiano ya 2003 ya UNESCO yalichangia ule utashi wa kutafuta majukumu mapya ya maakaba hizi zaidi ya yale yao ya kiasili katika mawanda ya utafiti na elimu. Vitu kutoka katika maakaba hizi sasa vinatu-miwa kuhuisha muziki na asili za ngoma katika jamii husika.

Taasisi ya Muziki ya Akademia ya Hungary ikishirikiana na akademia zingine za Ulaya inatayarisha mradi uitwao “*Open Musical Archives on the Internet*” (Maakaba wazi za Muziki kwenye Mtandao wa Mawasiliano) ili kuupa umma nafasi huru na rahisi ya hazina data za muziki na ngoma. “Bartók System” (Utaratibu wa Bartók) pekee ambayo ni sehemu ya tovuti ya taasisi hiyo ina takriban nyimbo 14,000 za kiasili pamoja na habari zingine muhimu zilizokusanywa na Béla Bartók, Zoltán Kodály wakishirikiana na wenzao, pamoja na waliowarithi kati ya 1896 na 1940. Hazina data ya “Musical Sound Publications” (Machapisho ya Sauti za Muziki) iliyo katika tovuti hiyo ina idadi nyingine ya nyimbo 6,000 za kiasili na lahani zilizochapishwa kwenye rekodi za ngozi ya plastiki, kwenye maumbo ya mashine za umeme au maumbo mengine ya mawasiliano kati ya 1950 na 2000. Aidha, kifaa mahsusi kimechopeka kwenye injini ya hazina data ili kuzisaidia jamii kupata maumbo ya muziki kutoka katika maeneo yao. Wageni wanaotembelea tovuti hiyo wanaweza kusikiliza au kupakua maumbo yote haya ya muziki. Hazina data zilizoko kwenye mtandao wa mawasiliano hupokea wageni wengi kutoka katika jamii mbalimbali ambazo sasa zinaingiza hifadhi hizi za muziki kwenye mitaala ya elimu na programu za kitamaduni. Kwa upande wao, jamii hutoa hifadhi mpya za mapokezi za kisasa.



© Abu Dhabi Authority for Culture and Heritage (ADACH)





© Veli J. Sumingait

*(Juu) Mwanamume wa Kisubanen (Ufilipino) akifanya tambiko kabla ya kuingia katika eneo fulani huku akiomba ruhusa kutoka kwa asiyeonekana ili kupata maandiko*

*(Kulia) Ma Quang Chong na Ma Quang Eng wakijifunza kuendesha vikaragosi vya fito katika Kijiji cha Tham Roc.*



La Cong Y. © Vietnam Museum of Ethnology

## UFILIPINO: Maandiko ya Hifadhi yanayohusisha Jamii Yanachangia Kufanikisha Turathi za Tamaduni Zisizogusika

Kati ya 2003 na 2004, jamii ya Subanen iliyoko Magharibi mwa Mindanao huko Ufilipino ilianzisha maandiko ya kuhifadhi ujuzi wao wa kiasili kuhusu mimea ambayo inapatikana katika maeneo yao ya kiasili. Mimea hiyo ni muhimu kwao kwa sababu za kimatibabu, kilimo, kiuchumi na kidini.

Uanuwai wa mimea katika eneo hilo sasa unapungua kwa sababu ya wingi wa watu pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa. Wavyele walitambua kuwa uanuwai wa mimea unapodidimia, ujuzi wao wa mimea pia unapungua. Walitambua pia kwamba kizazi kipya kinakumbatia jamii pana, na ule ujuzi wa kiasili unaopitishwa kwa njia ya mdomo haupitishwi tena kwa kizazi kinachofuata, na hivyo unaweza kupotea kabisa.

Viongozi wa Subanen walitafuta usaidizi kutoka katika mashirika ya kitaaluma ili yawasaidie kupata maarifa ya kuweza kuhifadhi wenyewe kimaandishi ujuzi huu wa kiasili, wakisaidiwa na wataalamu kutoka nje. Wazee wa jamii hii ambao hawajui kusoma na kuandika lakini wenye ujuzi mwingi, walitoa habari huku kizazi kipya kikiwa waandishi.

Maandishi hayo yalihifadhiwa katika maumbo mbalimbali ya mawasiliano kwa lugha ya Kiingereza kukiwemo na tafsiri za Kisubanen. Ili kulinda hati miliki za jamii, kazi hizi zilisajiliwa kupitia kwa afisi ya serikali ya hati miliki. Programu ya elimu katika jamii hii sasa hutumia kazi hizo kufundisha watoto wa shule utamaduni wao; hutumiwa pia kama kazi za mitaala kwa watu wazima wanaotaka kujifunza kusoma na kuandika katika lugha yao ya kiasili.

Maandiko haya yaliyofanywa na jamii yenyewe yamefaulu kama njia moja ya kuhifadhi ujuzi wa jamii na mimea kupitia masimulizi ya mdomo na kuuwezesha ujuzi huu kupatikana miongoni mwa vizazi vya sasa na vijavyo huku ukichangia katika kudumishwa kwa Turathi za Tamaduni Zisizogusika katika jamii ya Subanen.



© Veli J. Sumingait

## VIETNAM: Kuandika na Kuhuisha Ufundi wa Kucheza Karagosi

Pamoja na ishara ya uchezeshaji vikaragosi majini, Viet Nam ina idadi isiyojulikana sana katika mila yao ya kucheza vikaragosi kwa kutumia fito miongoni mwa watu wa Tay kutoka katika kijiji cha Tham Roc kwenye jimbo la Thai Nguyen, kaskazini mwa Hanoi. Kwa kipindi cha vizazi vitano vilivyopita, wachezeshaji vikaragosi walikuwa hawajafanya hivyo kwa miongo mingi mpaka wakati makavazi ya Ethnolojia ya Viet Nam ilipoanzisha uchezeshaji vikaragosi katika kusanyiko lake la mwaka wa 1997. Wakiwa wamehamasishwa na hatua hii, wanakijiji kutoka Tham Roc walianza kujiliza ikiwa wangeweza kuona uchezeshaji wa vikaragosi tena.

La Cong Y aliyekuwa mtafiti wa makavazi kutoka katika jamii ya Tay alipendekeza idara ya vielelezo vya kusikia na kuona kutayarisha filamu ya ethnografia kuhusu mila hiyo. Makavazi ilichangia katika kutafuta usaidizi wa kifedha kutoka katika afisi ya Shirika la Ford Foundation iliyoko Hanoi. Wafanyi kazi wa makavazi walipewa mafunzo ya kuweka hifadhi ya nyaraka kwa kutumia video na pia kuhariri. Kikundi hicho kilienda kufanya kazi Tham Roc kwenye mwaka wa 1999.

Kizingiti kikubwa walichokumbana nacho ni kwamba wanakijiji hawakuwa wanacheza vikaragosi kwenye maonyesho tena. Walikuwa wameikataa mila hii na kuichukulia kama dalili ya ushirikina hasa katika nyakati za mapinduzi ya miaka ya 1950. Kwa bahati nzuri, walikuwa wameweka vikaragosi ndani ya masanduku wakayahifadhi kwenye pau za nyumba ya mzee wa kijiji. Wahudumu wa mila hiyo waliwaeleza watayarishaji filamu kwamba wanakijiji hawakuwa tayari kutoa vikaragosi kwa sababu walezi wa kiroho wa vikaragosi hivyo wangeweza kukasirika. Serehe mahsus zilihita kufanywa kabla ya wao kufungua masanduku na kucheza vikaragosi tena.

Huku kamera zikirekodi, vikaragosi vilitolewa nje na kuendesha. Video ya kiethnografia ilihitaji upeo wa simulizi, na hili lilitimia wakati wa mchezo wa vikaragosi vya watu wa Tay kutoka Tham Roc baada ya miongo mingi. Wanakijiji walianza kazi kwa ushupavu, huku mababu wakiwafunza wajukuu wao wa kiume, na kwa mara ya kwanza wajukuu wa kike, jinsi ya kuendesha vikaragosi huku wakirejelea matini za zamani. Ugizaji uliorekodiwa kwa ajili ya makavazi haukuwa wa mwisho. Kwa sababu walihamasishwa kutokana na mafanikio ya video, wachezeshaji vikaragosi wa Tham Roc wameendelea kufanya maonyesho mara kwa mara katika jimbo lao na katika makavazi ya Ethnolojia huko Hanoi. Kama alivyosema mkurugenzi wa makavazi wa awali, Nguyen Van Huy, "Ujuzi wa kiasili ulioko katika kutengeneza na kucheza vikaragosi umeanzishwa upya...na ule mshikamano wa jamii ulipata nguvu" – yote haya kupitia mradi wa kuhifadhi nyaraka.

*Mmoja wa kundi la kuhifadhi nyaraka la Subanen akipokea habari kutoka kwa mzee katika jamii hiyo.*

**MCHAPISHAJI** Idara ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika (ITH)  
Sekta ya Tamaduni, UNESCO  
1 Rue Miollis  
75732 Paris Cedex 15, Ufaransa  
Barua pepe: ich@unesco.org  
Kipepesi: +33 (0) 145685752

**MHARIRI MKUU** Rieks Smeets

**JOPO LA UHARIRI** Estelle Blaschke, Frank Proschan,  
David Stehl, Samantha Wauchope,  
Reiko Yoshida


**MWANA-RUWAZA** Jean-Luc Thierry

**Tolea la Messenger kuhusu Turathi Zisizogusika** linapatikana katika umbo la chapa na elektroniki kwa Kiingereza, Kifaransa, Kihispania na Kiarabu.

Nakala ya Kiarabu imezeweshwa kupitia kwa mchango wa kifedha wa Mamlaka ya Utamaduni na Turathi ya Abu Dhabi, Milki ya Abu Dhabi – U.A.E.

Yote yaliyomo yanaweza kupakuliwa katika ([www.unesco.org/culture/ich](http://www.unesco.org/culture/ich)) na kupigwa chapa bila malipo ilimradí mwandishi atambuliwe.

© Conselho das Ateleias Waijipi-Apina



# turathi zisizogusika

## KALENDA

- MEI 23-27** Kikao cha kwanza kisichokuwa cha kawaida cha Kamati maalumu kati ya serikali za Mataifa Wanachama ya Hifadhi za Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Chengdu, Uchina.
- MEI 23–JUNI 10** Maonyesho ya Picha: “Turathi-Hai: Kuchunguza Zisizogusika” katika Bustani ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika ya *Theme Park* wakati wa sherehe za kimataifa kuhusu Turathi za Tamaduni zisizogusika. Chengdu, Uchina.
- JUNI 11-14** Majadiliano ya pamoja ya lugha zinazohatarishwa na masimulizi ya kiasili. Havana, Cuba.
- SEPTEMBER 3-7** Kikao cha pili cha kawaida cha Kamati ya serikali za nchi kuhusu kuhifadhi Turathi za Tamaduni Zisizogusika. Ujapani.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na: [ich@unesco.org](mailto:ich@unesco.org)



*Papi za Picha kwenye Barabara ya Ségur.*

## PAPUA NEW GUINEA: Thamani ya Rekodi za Zamani Wakati wa Sasa

Mwishoni mwa miaka ya 1990, Akademia ya Sayansi ya Austria mjini Vienna ilishirikiana na Taasisi ya Papua New Guinea ili kukusanya rekodi za sauti kwenye maakaba yake ya sauti ambayo inaweza kupatikana popote. Katika mwaka wa 2000, Akademia hiyo ilichapisha SIDII tano za muziki, masimulizi ya hadithi na maumbo mengine ya kiisimu. Kadhalika, kuna SIDII inayowasilisha ukusanyaji wa maandishi wa awali, ikiwemo chapa ya tafsiri kwa Kiingereza yenye kurasa 223. SIDII hii ambayo pia ilifanyiwa marekebisho upya ina habari muhimu za wakusanyaji na umuhimu wao\* (<http://www.oew.ac.at/verlag>).

Mambo mengi yalikusanywa na mwana anthropolojia wa Austria Rudolf Pöch, ambaye aliyakusanya kutoka katika maeneo matatu tofauti ya New Guinea tokea mwaka wa 1904 hadi 1906. Pia kuna rekodi zilizo hifadhiwa tangu mwaka wa 1907 ambazo zilikusanywa Ulaya na kijana wa Papua New Guinea na kutayarishwa na Fr. Wilhelm Schmidt. Zingine zilitarishwa Papua New Guinea kati ya 1908-9 na Fr. Josef Winthuis, ambaye alikuwa Mmisheni wa kwanza kuweka rekodi za maandishi ya nyanjani nchini humo. SIDII iliyotayarishwa ilisambazwa kwenye taasisi na vituo vya utamaduni nchini, ambapo pia utambuzi wa umma kuhusu mambo haya ulikuzwa kupitia kwa magazeti na vituo vya redio nchini.

Ni watu wachache ambao walijua kuwepo kwa rekodi hizi za kihistoria. Hivyo, matumizi yake yalikuwa madogo, sembuse haja ya kuzitumia. Katika nyakati za hivi karibuni, wana isimu na wana taaluma ya muziki wamefaidika kutokana na kulinganisha rekodi hizo na desturi za kisasa. La muhimu hapa ni ile rekodi ya kwanza ya maandishi ya pijini ijulikanayo kama Tok Pisin nchini Papua New Guinea, ambayo sasa ni lugha inayozungumzwa na wengi nchini. Baadhi ya rekodi hizo zilikusanywa maandiko ya nyimbo za sherehe ambazo sasa hazichezwi – zilikatazwa na Wamisheni au pia mahali pa nyimbo hizo kuchukuliwa na sherehe kutoka kwa makundi jirani. Mila kama hizo sasa hukumbukwa kupitia maumbo finyu tu. Huku zikihimiliwa na picha zilizopigwa wakati wa utafiti wa nyanjani, rekodi hizi za maandishi pia zinathibitisha desturi za michezo ya kisasa, na hivyo kutoa thibitisho la kimaandishi kwamba baadhi ya mila na desturi za wenyeji bado zinaendelezwa kupitia kwa michezo hiyo ya kisasa. Kwa sababu baadhi ya majina ya waimbaji yamerekodiwa, leo wanajamii wanaweza kusikia sauti za wavyele wao. Makundi ya wachezaji wa kiasili sasa yanatumia rekodi hizi ili kuwahamasisha wazee wa kijiji kukumbuka desturi za michezo ya ujana wao, ambazo pia zinaweza kupitishwa kwa vizazi vichanga. Bila kuwa na rekodi hizi kama vianzio, uhuishaji wa desturi na mila hizi hautawezekana.

Rekodi za zamani zilizo hifadhiwa upande mwingine wa dunia zina umuhimu mkubwa kwa Papua New Guinea ya leo. Huzungumzia juu ya desturi ambazo zingekuwa zimepotea, na kuthibitisha upya kuwepo kwa mila zao za kiasili. Wale waliorekodiwa huenda walikwisha kufariki zamani, lakini sauti zao zinaendelea kuvipa msukumo vizazi vipya kwa namna nyingi.

\* *Tondokumente aus dem Phonogrammarchiv der Österreichischen Akademie der Wissenschaften. Gesamtausgabe der historischen Bestände 1899–1950. Series 3: Papua New Guinea (1904–1909).* Dietrich Schüller (ed.), commentary by Don Niles (<http://www.oew.ac.at/verlag>).

## Tembelea Kituo cha Habari za Turathi za Tamaduni Zisizogusika!

Mwisho wa mwaka wa 2006 ulishuhudia kufunguliwa kwa kituo cha habari za turathi za tamaduni zisizogusika katika orofa ya tisa ya jumba la UNESCO la Bonvin. Kituo hiki cha habari hutoa aina mbalimbali za machapisho (tokea kurasa zenye matangazo hadi tasnifu za uzamifu), picha na rekodi za video na aina mbalimbali za vifaa vya mawasiliano ambavyo vinaweza kutumiwa papo hapo. Kituo kinafanya kazi ili kujumuisha pamoja habari zinazohusu shughuli za awali za UNESCO, hususan zile za nyanjani katika mawanda ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika, zikiwa ni pamoja na maandiko juu ya Vito vitatu vya thamani. Kituo kitajumuisha pia kwa njia hiyo, matayarisho na utekelezaji wa Maafikiano ya 2003. Aidha, kinatarajia kukusanya machapisho na data zingine zozote zinazohusiana na ulinzi wa turathi za tamaduni zisizogusika kote ulimwenguni. Kwa hakika, kituo hiki cha habari ni maakaba ya Afisi ya Utawala ya Maafikiano.

Tuna furaha kupokea na kuwasilisha habari zozote za Turathi za Tamaduni Zisizogusika, pamoja na hatua za kuhifadhi turathi hizo ambazo wizara, mashirika yasiyokuwa ya serikali, jamii mbalimbali na watafiti wangependa kutuletea. Kwa sababu nafasi katika chumba cha kusomea haitoshi, wageni wanaombwa kuwasiliana na kituo hiki ili kupanga tarehe ya kuzuru. Kituo hufunguliwa kwa umma kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa kati ya saa 8.30 mchana hadi saa 12 jioni; asubuhi ni kupitia kupanga na kituo wakati wa kuzuru.

**Anwani:** ICH Information Centre – Office B 9.25  
1 rue Miollis, 75015 Paris (métro Ségur)

**Wasiliana na:** Bw. Ronan Grippay  
Simu: +33(0)1 45 68 44 39  
Barua pepe: [r.grippay@unesco.org](mailto:r.grippay@unesco.org)